ISSN 0856 – 034X

*Supplement No. 29* *22nd July, 2022*

# *SUBSIDIARY LEGISLATION*

*to the Gazette of the United Republic of Tanzania No. 29 Vol. 103 dated 22nd July, 2022*
*Printed by the Government Printer, Dodoma by Order of Government*

TANGAZO LA SERIKALI NA. 503 la tarehe 22/7/2022

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA,

(SURA 290)

## SHERIA NDOGO

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 6(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO ZA ADA NA USHURU ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA ZA MWAKA 2022.

### SEHEMU YA KWANZA

### MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela za Mwaka 2022

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo:-

"Ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni zitolewazo na Halmashauri;



Scanned with CamScanner

"Afisa mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"chombo cha usafiri" maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha mtu, watu au mizigo kutoka sehemu moja kwenda nyingine isipokuwa mkokoteni au wanyama wanaotumika kusafirisha watu au mizigo;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela.

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri ;

"machinjio" maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama na kuanika ngozi;

"madini ya ujenzi" maana yake ni mchanga, mawe, moramu, vumbi la kokoto, kokoto, udongo, matofali ya kuchoma au mabichi na chokaa;

"maegesho'' maana yake ni sehemu yeyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha chombo cha usafiri kwa muda;

"mhudumu" maana yake ni mtu yeyote anayehudumia wateja katika eneo la biashara;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela au afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

"*usajili wa vyombo vya usafiri*" maana yake ni utaratibu uliowekwa na Halmashauri wa kuorodhesha na kutambua idadi ya vyombo vya usafiri vinavyofanya biashara ndani ya mamlaka ya Halmashauri;

"ushuru" maana yake ni malipo yanayofanywa kwa Halmashauri au wakala wake kwa ajili ya huduma inayotolewa na Halmashauri;

"ramani ya jengo" maana yake ni mchoro au michoro inayotakiwa kuwasilishwa Halmashauri chini ya Kanuni za udhibiti wa maendeleo ya ujenzi mijini;

"soko" maana yake ni sehemu yoyote maalum iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuuza na kununua bidhaa;

"Wakala" maana yake ni mtu, taasisi, kampuni au Asasi yeyote iliyoteuliwa kisheria na Halmashauri kukusanya mapato kwa niaba ya Halmashauri;

"Kituo cha Mabasi' maana yake ni eneo lililotengwa kwa ajili ya kushusha na kupakia abiria ndani na nje ya Halmashauri.

"Kituo cha malori" maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kupakia na kushusha mizigo.

"Kituo cha daladala" maana yake ni eneo lililotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kushusha na kupakia abiria.

SEHEMU YA PILI
NAMNA YA KUKUSANYA ADA NA USHURU

Ada na Ushuru

4. (1) Halmashauri itatoza ada na ushuru mbalimbali kwa ajili ya vibali, leseni na huduma zitolewazo na Halmashauri kama inavyoonyeshwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria ndogo hizi.

(2) Ushuru utozwao chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kabla ya kupata huduma.



Scanned with CamScanner

(3) Chombo cha usafiri au cha kubebea mazao au bidhaa kitakachokuwa kimebeba aina tofauti ya mazao au bidhaa kitatozwa ushuru kwa kiwango cha zao au bidhaa moja yenye kiwango kuliko vingine vilivyomo kwenye chombo husika.

(4) Huduma zitakazotozwa ada na ushuru katika Sheria Ndogo hizi ni;

(a) ada za vibali vya ujenzi
(b) ada ya kubadili matumizi ya ardhi
(c) ada za uthamini na upimaji ardhi;
(d) ada ya upimaji wa afya;
(e) ushuru wa machinjio;
(f) ushuru wa kulaza mifugo machinjioni;
(g) ada ya ukaguzi wa afya ya mnyama kabla ya kuchinjwa;
(h) Ada ya ukaguzi wa nyama kuruhusu kwenda buchani;
(i) Ushuru wa kuruhusu kuingiza wanyama na nyama iliyochinjwa nje ya Halmashauri;
(j) ada ya ukaguzi wa mazao mengine ya mifugo;
(k) ada ya huduma nyingine za mifugo;
(l) ushuru wa madini ya ujenzi;
(m) ushuru wa kushusha na kupakia mazao katika maeneo ya umma na binafsi
(n) ushuru wa kushusha na kupakia mazao ya misitu
(o) ushuru wa kushusha na kupakia bidhaa za viwandani katika maeneo ya umma na binafsi;
(p) ushuru wa kushusha na kupakia mazao na bidhaa mchanganyiko katika maeneo ya masoko na stendi;
(q) ushuru wa kituo cha mabasi



Scanned with CamScanner

Buzuruga;

(r) ushuru wa Kituo cha mabasi Nyamhongolo;

(s) ushuru wa kupaki malori Nyamhongolo;

(t) ada ya vyumba vya kulala wageni Stendi ya Nyamhongolo;

(u) ada ya choo cha umma Nyamhongolo stendi.

(v) ada ya kupangisha majengo ya Halmashauri;

(w) ada ya kupangisha vyumba/ vibanda/meza/vizimba vya biashara;

(x) ada ya kupangisha vyumba vya biashara stendi ya Nyamhongolo;

(y) ada za vibali vya burudani na michezo;

(z) ada kwa huduma za mzani;

(aa) ushuru wa maegesho kwenye maeneo maalum;

(bb) ushuru wa kituo vya kuosha vyombo vya usafiri;

(cc) ushuru wa viwanda vya kutengeza tofali;

(dd) ushuru wa vituo vya kutengeneza samani;

(ee) ushuru wa gereji;

(ff) ada ya usajili wa kikundi cha kijamii;

(gg) ushuru wa samaki na mazao ya ziwani;

(hh) ada ya kusajili taxi za mtandaoni;

Wajibu wa kulipa ada na ushuru

5. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayetakiwa kulipa ada na ushuru kuhakikisha kwamba analipa kwa viwango vilivyoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) muda wa kukusanya ushuru utakuwa ni kwa masaa yote



Scanned with CamScanner

ishirini na nne kila siku.

(3) Malipo ya ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yeyote itakayokubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na mlipa ushuru.

(4) Malipo ya Ushuru yanayotozwa kwa Mujibu wa Sheria Ndogo hizi yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake na kutolewa stakabadhi ya Halmashauri kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

Mabadiliko ya viwango vya ada na ushuru

6. (1) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kufanya marekebisho ya viwango vya ada na ushuru pale itakapoona inafaa kuendana na bei ya soko.

Sura 288

(2) Katika kufanya marekebisho ya viwango vya ada na ushuru au kipengele chochote katika Sheria Ndogo hizi, Halmashauri itafuata taratibu zote za utungaji wa Sheria Ndogo zinazoelekezwa na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji).

Usimamizi wa sheria ndogo

7. (1) Halmashauri inaweza kufunga biashara au kusimamisha uendeshaji wa shughuli yoyote ambayo itafanyika bila ya kuwa na leseni au kutokuwa na kibali kinachotolewa na Halmashauri.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri au Wakala wake anaweza kukamata na kuzuia mali au bidhaa za mtu yeyote ambaye ameshindwa kulipa kwa mujibu wa masharti ya Sheria Ndogo hizi.

(3) Endapo mmiliki wa mali au bidhaa iliyokamatwa kwa mujibu wa aya ndogo ya (2) atashindwa kulipa ushuru unaodaiwa ndani ya siku saba kwa mali au bidhaa zisizoharibika haraka na ndani ya siku mbili kwa mali au bidhaa zinazoharibika haraka, Halmashauri, baada ya kupata amri ya Mahakama, itakuwa na mamlaka ya kuuza mali au bidhaa na fedha zitakazopatikana zitarejeshwa kwa mmiliki wa mali au bidhaa hizo baada ya kutoa ada au ushuru unaodaiwa, gharama za kuhifadhi mali au bidhaa gharama za mahakama na gharama za mnada.

(4) Wakala anaruhusiwa kukamata mali au bidhaa bila kupata



Scanned with CamScanner

idhini ya maandishi ya Mkurugenzi.

(5) Halmashauri haitawajibika kwa uharibifu wa bidhaa au mali iliyokamatwa chini ya kifungu hiki isipokuwa tu kama uharibifu huo utakuwa umesababishwa na Halmashauri.

Uteuzi wa Wakala

8. Halmashauri inaweza kuteua kampuni, asasi au taasisi yoyote kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika vyanzo vilivyokubaliwa kukusanywa na Wakala.

Wajibu wa wakala

9. Wakala aliyeteuliwa chini ya Sheria Ndogo hizi atakuwa na wajibu wa-

(a) kukusanya au kupokea Ushuru katika eneo na chanzo alichopangiwa kwa viwango vilivyoainishwa chini ya Sheria Ndogo hizi;

(b) kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala kati yake na Halmashauri;

(c) kuweka dhamana ya kusanyo la miezi mitatu kabla ya kuanza kukusanya ambapo dhamana hiyo itarejeshwa mwisho wa mkataba.

Uwezo wa Afisa mwidhiniwa

10. Afisa mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa : -

(a) kuingia katika jengo lolote kwa lengo la kukukusanya ushuru;

(b) kukagua eneo au chombo chochote atakachokitilia mashaka kuwa kinahifadhi au kusafirisha bidhaa au kinatumika kukwepa kulipa ushuru; na

(c) kufunga biashara au jengo lolote ambalo mmiliki wake atashindwa au kukataa kulipa Ada au Ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Katazo la kufungua mwalo

11. (1) Hairuhusiwi kwa mtu yeyote kufungua mwalo wa mazao ya uvuvi sehemu yoyote ndani ya maeneo ya



Scanned with CamScanner

Halmashauri.

(2) Ikiwa mtu yeyote atafungua mwalo, kugoa, au kuegesha chombo cha uvuvi au usafirishaji mizigo au abiria ziwani kwenye mwalo usio rasmi atakuwa ametenda kosa.

(3) Vyombo vyote vinavyofanya shughuli za uvuvi au usafirishaji ndani ziwa Victoria vitalazimika kulipa ada stahiki na ushuru wa kuegesha pembezoni mwa ziwa au majini kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

## SEHEMU YA III
## MAKOSA NA ADHABU

Makosa katika mwalo wa kirumba

12. (1) Mtu yeyote atakayegonga jengo, geti, kingo za mzani na aina yoyote ya uharibifu atakuwa ametenda kosa na atawajibika kugharamia matengenezo yatakayotokana na uharibifu huo chini ya usimamizi wa mhandisi wa Manispaa.

(2) Mtu yeyote atakayepakia samaki au mazao yeyote ya uvuvi nje ya maeneo rasmi yaliyobainishwa na Halmashauri atakuwa ametenda kosa.

(3) Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kupakia mzigo wa mazao ya uvuvi bila kupima uzito wa gari kabla na baada ya kupakia.

Makosa ya jumla

13. Itakuwa ni kosa chini ya Sheria ndogo hizi;

(1) Kwa wakala yeyote

(a) kukusanya ushuru bila kibali cha maandishi au mkataba kutoka kwa Halmashauri;

(b) kukusanya au kujaribisha kukusanya ushuru kwa kiwango tofauti na kilichotajwa kwenye Sheria ndogo hizi;

(c) kushindwa kuwasilisha au kuwasilisha kiwango pungufu ya kiwango cha ushuru alichokubaliwa katika mkataba;



Scanned with CamScanner

(2) Kwa mtu yeyote endapo;

(a) atashindwa, atadharau, au atakaidi au atakataa kulipa ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kuhusiana na ulipaji wa ushuru chini ya Sheria ndogo hizi;

(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukataa au kukwepa kulipa ushuru;

(c) atatengeneza, atatayarisha, ataidhinisha utengenezaji au atatunza nyaraka za uongo kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa ushuru mbalimbali ndani ya Halmashauri;

(d) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri, au atashindwa au kutoa taarifa zitakazohitajika na Halmashauri;

(e) atashindwa kuweka kumbukumbu, vitabu, hesabu, au maelezo yoyote yatakayohitajika Halmashauri; na

(f) atamzuia Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake.

Adhabu ya jumla

14. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili (12) na kisichozidi miezi ishirini na nne (24) au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufililisha kosa

15. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini ya shilingi laki mbili iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari yake mwenyewe kwa maandishi na kukubali kutekeleza wajibu wake pamoja na kulipa faini anayodaiwa kama ilivyoekelezwa katika Jedwali la Pili la Sheria ndogo hizi.



Scanned with CamScanner

Kufuta TS Na. 278 la mwaka 2019

16. Sheria Ndogo hizi zimefuta Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, 2019.

---

JEDWALI LA KWANZA

---

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(1))*

1. ADA YA VIBALI VYA UJENZI

| Na. | AINA | KIWANGO |
|---|---|---|
| 1 | Majengo ya Makazi | |
| | i. Jengo la kawaida | 100,000/= |
| | ii. Jengo la ghorofa moja | 150,000/= |
| | iii. Jengo la ghorofa mbili | 200,000/= |
| | iv. Jengo la ghorofa tatu | 250,000/= |
| | v. Jengo la ghorofa nne | 300,000/= |
| | vi. Jengo la ghorofa tano na kuendelea. | 400,000/= |
| 2 | Majengo ya Biashara | |
| | i. Jengo la kawaida | 120,000/= |
| | ii. Jengo la ghorofa moja | 200,000/= |



Scanned with CamScanner

| | | |
|---|---|---|
| | iii. Jengo la ghorofa mbili | 500,000/= |
| | iv. Jengo la ghorofa tatu | 600,000/= |
| | v. Jengo la ghorofa nne | 700,000/= |
| | vi. Jengo la ghorofa tano na zaidi | 800,000/= |
| 3 | Kituo cha Mafuta | 2,000,000/= |
| 4 | Hotel, nyumba ya kulala wageni au ukumbi | 500,000/= |
| 5 | Taasisi, makanisa au msikiti<br>i. Jengo la kawaida<br>ii. Ghorofa | <br>200,000/=<br>300,000/= |
| 6 | Viwanda<br>i.Kiwanda kidogo<br>ii. Kiwanda cha kati<br>iii.Kiwanda kikubwa | <br>200,000/=<br>300,000/=<br>500,000/= |
| 7 | Kuongeza jengo | 50% ya gharama za kibali cha awali |
| 8 | Kubadili jengo | 50% ya gharama za kibali cha awali |
| 9 | Mnara | 2,000,000/= |
| 10 | Kupangisha ardhi kwa matumizi ya minara ya mawasiliano | 500,000/= |
| 11 | Ujenzi wa uzio wa muda | 500/= kwa kila mita moja kwa muda wa miezi 12 |
| 12 | Ujenzi wa uzio wa kudumu (makazi) | 1,000/= kwa kila mita moja |
| 13 | Ujenzi wa uzio wa kudumu (biashara) | 1,200/= kwa kila mita moja |
| 14 | Maombi ya uwekaji wa bango (bunners, installation fee) | 20,000/= kwa kila mita ya ujazo kwa mwezi |
| 15 | Pango la kutumia eneo la barabara (Buffer zone) au eneo la wazi la kibiashara kwa majengo yasiyo ya kudumu | 5,000 kwa kila mita moja ya Mraba kwa kila mwezi |
| 16 | Kupangisha maeneo ya wazi kwa majengo yasiyo ya kudumu na yanayohamishika | Tsh.5,000/= kwa kila mita moja ya mraba kwa |



Scanned with CamScanner

| | | |
|---|---|---|
| | | kila mwezi |

2. ADA NA VIBALI VYA KUBADILISHA MATUMIZI YA ARDHI, KUGAWA VIWANJA, MASHAMBA AU KUREKEBISHA MCHORO

| | Matumizi ya Awali | Matumizi yanayoombwa | Kiwango cha Ada |
|---|---|---|---|
| 1 | Makazi pekee | Makazi na biashara | 150,000/= |
| 2 | Makazi pekee | Makazi zaidi ya moja (apartment) | 100,000/= |
| 3 | Makazi pekee | Shule,hosteli,zahanati na huduma nyinginezo za jamii | 200,000/= |
| 4 | Makazi pekee | Hoteli | 200,000/= |
| 5 | Makazi na biashara | Kituo cha mafuta | 250,000/= |
| 6 | Makazi na biashara | (Maduka makubwa ) Super Market/Shooping Mall | 300,000/= |
| 7 | Makazi pekee | (Viwanda/huduma) Service Trade/Industrial | 200,000/= |
| 8 | Makazi pekee | Ghala (Yard/Godown) | 200,000/= |
| 9 | Biashara | Makazi | 100,000/= |
| 10 | Kugawa shamba kuwa viwanja vya makazi | Makazi | 10,000/= kwa kila kiwanja. |
| 11 | Kugawa kiwanja cha makazi | makazi | 100,000/= |
| 12 | Kugawa kiwanja kwa matumizi ya hoteli | biashara | 200,000/= |
| 13 | Kugawa kiwanja kwa matumizi ya shule, hosteli, zahanati na huduma nyinginezo za jamii. | Biashara | 100,000/= kwa kila ekari moja |
| 14 | Ada ya uhakiki wa umiliki kiwanja au shamba (Official Search) | matumizi yoyote | 50,000/= |



Scanned with CamScanner

3. ADA YA KUFANYA UTHAMINI NA UPIMAJI

| Na | AINA YA MATUMIZI YA KIWANJA | KIASI KWA KILA |
|---|---|---|
| 1 | Makazi pekee | 100,000/= |
| 2 | Makazi na biashara | 100,000/= |
| 3 | Biashara pekee | 200,000/= |
| 4 | Kuomba kuhakikiwa mipaka ya kiwanja | 150,000/= |
| 5 | Kulipia ada ya gharama za upimaji | 200,000/= |
| 6 | Gharama kuomba nakala na ramani | 200,000/= |

4. ADA YA UPIMAJI WA AFYA

| Na | Ada husika | Kiwango cha Ada |
|---|---|---|
| 1 | Homa ya manjano katika masaa ya kawaida. | |
| | (a) Raia | 7,000/= |
| | (b) Mgeni | 10,000/= |
| | (c) Vipimo vya afya kwa watumishi wa hoteli, bucha na maduka kila baada ya miezi sita | 10,000/= |
| | (d) Udhibiti wa wadudu waharibifu kwenye makazi ya kawaida ( kwa mita ya mraba) | 5,000/= |

5. USHURU WA MACHINJIO

| Na | Mnyama | Kiwango cha ushuru | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 3000/= | Kila ng'ombe mmoja |
| 2. | Mbuzi na kondoo | 1500/= | Kila mbuzi au kondoo mmoja |
| 3. | Nguruwe | 2000/= | Kila nguruwe mmoja |
| 4 | Kuku, bata, bata mziga, kanga | 200/= | Kila mfugo mmoja |

6. ADA YA KULAZA MIFUGO INAYOZURULA



Scanned with CamScanner

| Na | Mfugo | Kiwango cha Ushuru | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe, Punda | 10,000/= | Kwa kila mfugo mmoja. |
| 2. | Mbuzi, kondoo | 5,000/= | Kila mbuzi au kondoo mmoja |
| 3. | Nguruwe | 5,000/= | Kila nguruwe mmoja |

7. ADA YA UKAGUZI WA AFYA YA MNYAMA KABLA KUCHINJWA

| Na | Aina ya Mnyama | Kiwango cha Ushuru | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 1500/= | Kwa kila mnyama |
| 2. | Mbuzi, kondoo | 1000/= | Kwa kila mnyama |
| 3. | Nguruwe | 1000/= | Kwa kila nguruwe |
| 4. | Kuku, bata, bata mzinga | 200/= | Kwa kila mfugo mmoja. |

8. ADA YA UKAGUZI WA NYAMA ILI KURUHUSU KWENDA BUCHANI

| Na | Aina ya Mnyama | Kiwango cha Ushuru. | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 1500/= | Kwa kila mnyama |
| 2. | Mbuzi,kondoo | 500/= | Kwa kila mnyama |
| 3. | Nguruwe | 1000/= | Kwa kila nguruwe |

9. ADA NA USHURU WA KUIINGIZA WANYAMA NA NYAMA ILIYOCHINJWA NJE YA HALMASHAURI

| Na | Aina | Kiwango cha Ada/ Ushuru | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Kuingiza nyama yoyote | 100/= kwa kilo moja | Kwa kila mfugo |
| 2. | Kuingiza wanyama wa kufuga Ng'ombe, Farasi | 10,000/= | Kwa kila mfugo |



Scanned with CamScanner

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3. | Kuingiza nguruwe | 5,000/= | Kwa kila mfugo |
| 4 | Mbuzi/Kondoo | 3000/= | Kwa kila mfugo. |

10. ADA YA UKAGUZI WA MAZAO MENGINEYO YA MIFUGO

| Na | AINA YA ZAO | KIASI CHA USHURU |
|---|---|---|
| 1. | Maziwa ya ng'ombe na Mbuzi | 100 kwa kila lita moja |
| 2 | Ngozi aina zote | 200 kwa kila lita moja |

11. ADA YA HUDUMA NYINGINE ZINAZOHUSU MIFUGO

| Na | Aina ya mfugo | Kiwango |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya kuanzisha josho la mifugo kwa mwaka. | 30,000/= @kila josho |

12. USHURU WA MADINI YA UJENZI

| Na | Ukubwa wa gari | Kiwango cha Ushuru |
|---|---|---|
| 1 | Gari tani 3- 4.9 | 3000/= Kwa safari(trip) |
| 2 | Gari tani 5-10 | 4000/= Kwa safari(trip) |
| 3 | Gari tani 11.1 -17 | 5000/= Kwa safari(trip) |

13. USHURU WA KUPAKIA NA KUSHUSHA MAZAO

| Na | BIDHAA | KIASI CHA USHURU WA KUSHUSHA AU KUPAKIA |
|---|---|---|
| 1. | Nafaka aina zote gunia la kilo 50 hadi kilo 100 | 1,000/= |
| 2 | Mazao ya kunde aina zote gunia kilo 50 hadi kilo 100 | 1,000/= |
| 3 | Mazao ya Mizizi aina zote gunia kilo 50 hadi kilo100 | 1,000/= |
| 4 | Mazao mengineyo kilo 50 hadi kilo 100 | 1000/= |
| 6 | Tenga kubwa la nyanya | 2000/= |
| 7 | Matunda aina zote tani 1 hadi tani 3 | 20,000/= |
| 8 | Matunda aina zote tani 3.1 hadi Tani 5 | 30,000/= |
| 9 | Matunda aina zote tani 5.1 hadi Tani | 50,000/= |



Scanned with CamScanner

| | | |
|---|---|---|
| | 7 9 | |
| 10 | Matunda aina zote tani 8 hadi zaidi | 70,000/= |
| 11 | Tenga la kuku | 2000/= |
| 12 | Viungo vya mboga kilo 50 hadi kilo 100 | 1000/= |

14 USHURU WA KUSHUSHA NA KUPAKIA MAZAO YA MISITU

| Na. | AINA YAZAO | UJAZO | USHURU |
|---|---|---|---|
| 1. | Mkaa | Kila gunia moja | 1,000/= |
| 2 | Mirunda na mbao | Tani 1 hadi tani 3 | 20,000/= |
| 3 | Mabanzi na kuni | Tani 1 hadi tani 3 | 15,000/= |
| 4 | Mirunda na mbao | Tani 3.1 hadi tani 7 | 30,000/= |
| 5 | Mabanzi na kuni | Tani 3.1 hadi tani 7 | 20,000/= |
| 6 | Mirunda na mbao | Tani 7.1 hadi tani 10 | 50,000/= |
| 7 | Mabanzi na kuni | Tani 7.1 hadi tani 10 | 30,000/= |
| 8 | Mirunda na mbao | Tani 10.1 hadi tani 15 | 70,000/= |
| 9 | Mabanzi na kuni | Tani 10.1 hadi tani 15 | 40,000/= |
| 10 | Mirunda na mbao | Zaidi ya Tani 15 na kuendelea | 100,000 = |
| 11 | Mabanzi na kuni | Zaidi ya Tani 15 na kuendelea | 50,000/= |

15. USHURU WA KUSHUSHA NA KUPAKIA BIDHAA ZA VIWANDANI.

| Na. | AINA YA BIDHAA | GARI UJAZO (UKUBWA WA TANI) | GHARAMA ZA USHURU |
|---|---|---|---|
| 1. | Bidhaa za ujenzi | Tani 1 hadi Tani 5.9 | 15,000/= |
| | | Tani 6 hadi Tani 10.9 | 20,000/= |
| | | Tani 11hadi 15.9 | 30,000 = |
| | | Tani 15 na zaidi. | 50,000/= |
| 2. | Bidhaa za chakula | Tani 1 hadi Tani 5.9 | 15,000/= |
| | | Tani 6 hadi Tani 10.9 | 20,000/= |
| | | Tani 11hadi 15.9 | 30,000 = |
| | | Tani 15 na zaidi. | 50,000/= |
| 3 | Bidhaa za vinywaji ( beverages) | Tani 1 hadi Tani 5.9 | 15,000/= |
| | | Tani 6 hadi Tani 10.9 | 20,000/= |
| | | Tani 11hadi 15.9 | 30,000 = |
| | | Tani 15 na zaidi. | 50,000/= |
| 4 | Bidhaa za matumizi ya nyumbani | Tani 1 hadi Tani 5.9 | 15,000/= |
| | | Tani 6 hadi Tani 10.9 | 20,000/= |
| | | Tani 11hadi 15.9 | 30,000 = |
| | | Tani 15 na zaidi. | 50,000/= |
| 5 | Vifaa vinavyotumia umeme | Tani 1 hadi Tani 5.9 | 15,000/= |
| | | Tani 6 hadi Tani 10.9 | 20,000/= |
| | Vifaa vinavyotumia umeme | Tani 11hadi 15.9 | 30,000/= |
| | Vifaa vinavyotumia umeme | Tani 15 na zaidi. | 50,000/= |
| 6 | Bidhaa za mafuta ya magari, mitambo na gesi | Tani 1 hadi tani 6.9<br>Tani 7 hadi tani 15 | 10,000/=<br>20,000/= |



Scanned with CamScanner

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Zaidi ya Tani 15 | 30,000/= |
| 7 | Vyuma Chakavu | Tani 1-5.9 | 15,000/= |
| | Chuma chakavu | Tani 6-10.9 | 30,000/= |
| | Chuma chakavu | Tani 11-15.9 | 50,000/= |
| | Chuma chakavu | Tani 16 na zaidi | 100,000/= |

16. USHURU WA KUSHUSHA NA KUPAKIA MAZAO NA BIDHAA ZA VIWANDANI MCHANGANYIKO

| Na | AINA YA BIDHAA | USHURU |
|---|---|---|
| 1. | Bidhaa zilizobebwa kwenye bajaji | 3,000/= |
| 2 | Bidhaa zilizobebwa kwenye pikipiki ya miguu miwili | 1,000/= |
| 3 | Mafurushi makubwa ya bidhaa au mazao. | 1000 = |

17. USHURU WA MAGARI KITUO CHA MABASI BUZURUGA

| Na | Aina ya Gari | Kiwango cha Ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Abiria 1-18 | 1500/=kwa kila safari |
| 2 | Abiria 1-42 | 3000/=kwa kila safari |
| 3 | Abiria 1 -52 au zaidi. | 5,000/= kwa kila safari |
| 4 | Gari binafsi | 1000 kwa siku |
| 5 | Taxi | 1000 kwa siku |
| 6 | Bajaji | 500 kwa siku |
| 7 | Pikipiki | 500 kwa siku |

18. USHURU WA KITUO CHA MABASI NYAMHONGOLO

| Na | Aina ya Gari | Kiwango cha Ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Abiria 1- 18 | 1500/=kwa kila safari |
| 2 | Abiria 1-42 | 3000/=kwa kila safari |
| 3 | Abiria 1 -52 au zaidi. | 5,000 = kwa kila safari |
| 4 | Gari binafsi | 1000 kwa siku |
| 5 | Taxi | 1000 kwa siku |
| 6 | Bajaji | 500 kwa siku |
| 7 | Pikipiki | 500 kwa siku |

19. USHURU WA KUPAKI MALORI STENDI YA NYAMHONGOLO

| NA. | AINA YA HUDUMA | KIASI KWA SIKU |
|---|---|---|
| 1 | Kupaki lori | 2,000 = |

20. USHURU WA VYOO VYA UMMA NYAMHONGOLO STENDI

| Na | aina ya chanzo | aina ya huduma | Kiasi |
|---|---|---|---|



Scanned with CamScanner

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Choo cha stendi | haja ndogo | 300/= |
| | | haja kubwa | 300/= |
| 2 | Bafu la stendi | kuoga | 500/= |

21. ADA YA VYUMBA VYA KULALA WAGENI- NYAMHONGOLO – HOSTEL

| Na | AINA YA HUDUMA | KIASI KWA SIKU |
|---|---|---|
| 1. | Vyumba vikubwa | 25,000/= |
| 2. | Vyumba vya kawaida | 20,000/= |

22. ADA KUPANGISHA MAJENGO YA HALMASHAURI

| Na. | Nyumba | Ada ya Pango |
|---|---|---|
| 1. | Nyumba za kuishi zilizopo Kirumba | Tsh. 90,000 kwa mwezi |
| 2. | Ukumbi wa Halmashauri | Tsh. 500,000 kwa siku |
| 3. | Nyumba nyingine | Kwa mujibu wa mkataba |

23. ADA YA KUPANGISHA VYUMBA, VIBANDA, MEZA NA VIZIMBA VYA BIASHARA VYA HALMASHAURI

| Na. | SOKO | AINA YA PANGO | KODI KWA KILA MWEZI |
|---|---|---|---|
| 1 | BUZURUGA | i.vyumba vya mbele | 200,000/= |
| | | ii.vyumba vya ndani | 100,000/= |
| | | iii. Partition | 50,000/= |
| 2 | KIRUMBA | i.vyumba vya mbele | 60,000/= |
| | | ii.vyumba vya ndani | 50,000/= |
| | | iii. vizimba vya matunda | 9,000/= |
| | | iv. mgahawa | 60,000/= |
| | | v. ghala | 100,000/= |
| | | vi. Eneo la wazi | 5,000/= kwa $m^2$ kwa kila mwezi |
| 3 | KITANGIRI | i.vyumba vya mbele | 50,000/= |
| | | ii.vyumba vya ndani | 40,000/= |
| 4 | NYAMANORO | i.vyumba vya mbele | 50,000/= |
| | | ii.vyumba vya ndani | 40,000/= |
| 5 | MWALONI | i.meza | 50,000/= |



Scanned with CamScanner

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | ii.mgahawa | 20,000/= |
| | | iii.ofisi | 30,000/= |
| 6 | NYAKATO | i.vyumba vya mbele | 40,000/= |
| | | ii.vyumba vya ndani | 30,000/= |
| | | iii.vizimba vya mbao | 40,000/= |
| 7 | KILOLELI | i.vyumba vya mbele | 50,000/= |
| | | ii. vyumba vya ndani | 40,000/= |
| 8 | NYASAKA CENTRE | i.vyumba | 40,000/= |
| | NYASAKA NYANDA | i.nyanda | 40,000/= |
| 9 | SABASABA NAFAKA | i.meza za levmp&jengo la zamani | 10,000/= |
| | | ii.meza za kawaida | 9,000/= |
| | | iii. vyumba | 40,000/= |
| 10 | MSUKA | i.vyumba vya mbele | 60,000/= |
| | | ii. vyumba vya ndani | 50,000/= |
| 11 | KAWEKAMO | i.vyumba vya mbele | 60,000/= |
| | | ii. vyumba vya ndani | 50,000/= |

24. ADA YA KUPANGISHA CHUMBA CHA BIASHARA STENDI YA NYAMHONGOLO.

| Na. | AINA YA HUDUMA | KIASI KWA MITA MOJA YA MRABA KWA KILA MWEZI |
|---|---|---|
| 1. | Chumba cha duka | 25,000/= |
| 2. | Chumba cha benki | 50,000/= |
| 3. | Maduka makubwa (super markets) | 25,000/= |
| 4 | Maduka makubwa ya kati (min super markets) | 25,000/= |
| 5 | Restaurants (mgahawa mkubwa) | 25,000/= |
| 6 | Vyumba vya kukatia tiketi (booking rooms) | 30,000/= |
| 7 | Baa (bar) | 25,000/= |
| 8 | Eneo la kupumzikia abiria (Lounge for hire) | 20,000/= |
| 9 | Godoun (ghala la kuhifadhia mizigo) | 15,000/= |
| 10 | Gereji (workshop) | 10,000/= |
| 11 | Eneo la machinga | 5,000/= |
| 12 | Wauza vilainishi na spea za magari kwenye gereji | 10,000/= |

25. ADA NA USHURU UTOKANAO NA SHUGHULI ZA BURUDANI NA MICHEZO.

| Na | TUKIO LA BURUDANI | ADA/USHURU (Tsh) | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1 | Kibali cha tamasha;<br>lisilo na kiingilio | 100,000 | Ada zote ni kwa siku. |
| | Lenye kiingilio | 200,000 | |
| | Lenye kiingilio na matangazo | 400,000 | |
| 2 | Usajili wa vikundi vya sanaa, kwaya | Tsh 85,000 | Kwa usajili. |



Scanned with CamScanner

| | | | |
|---|---|---|---|
| | na kaswida | | |
| 3 | Kibali cha uandaaji kongamano | Tsh 80,000= | Kwa siku |
| 4 | Usajili wa vibanda vya filamu | Tsh 100,000/= | Kwa Mwaka |
| 5 | Kibali cha kuchezesha michezo ya kubahatisha kwa kutumia mashine | Tsh 20,000/= | Kwa kila mashine kwa Mwaka |
| 6 | Kibali cha mchezo wa pool table | Tsh 30,000/= | Kwa kila mashine/meza kwa Mwaka |
| 7 | Kibali cha tamasha la maonesho ( biashara) | Tsh 50,000/= | Kwa siku |
| 8 | Bahati nasibu ndogo ndogo ( fete) | Tsh 50,000/= | Kwa siku katika eneo moja |
| 9 | Msheherehaji | 50,000/= | Kwa tukio |
| 10 | Mpambaji wa ukumbi wa burudani (harusi, sherehe za jikoni, sherehe za kuaga binti na nyinginezo) | 50,000/= | Kwa tukio |
| 11 | Mtoa burudani ( D.J) | 50,000/= | Kwa tukio |
| 12 | Mmiliki wa kumbi mbalimbali | 50,000/= | Kwa tukio moja kwa siku |
| 13 | Mpishi wa vyakula | 50,000/= | Kwa tukio moja kwa siku. |
| 14 | Picha jongevu na mnato | 50,000/= | Kwa tukio moja kwa siku |
| 15 | Mnada wa hadhara | 50,000/= | Kwa tukio moja kwa siku. |
| 16 | Harusi za sherehe za kijamii | 50,000/= | Kwa tukio moja kwa siku |
| 17 | Ada ya Matangazo | | Ada zote kwa siku. |



Scanned with CamScanner

| | | | |
|---|---|---|---|
| | (a) Kibiashara na matangazo<br>(b) Yasiyo na biashara | (a) Kibiashara Tsh 200,000/=<br>(b) Yasiyo ya kibiashara Tsh 100,000/= | |
| 18 | Kukodi uwanja wa mpira furahisha | Tsh 100,000/= matukio yasiyo ya kibiashara au hayana ufadhili.<br>Tsh 200,000/= matukio ya kibiashara au yenye ufadhili. | Kwa siku moja tu. |

26. ADA YA HUDUMA ZA MZANI

| Na | HUDUMA | KIASI CHA ADA KWA KILA ANAPOPIMA |
|---|---|---|
| 1. | Kupima uzito wa gari kati ya tani 25-tan 35 | 15,000/= |
| 2. | Gari lenye uzito wa kati ya tan 12 -14 | 10,000/= |
| 3 | Gari lenye uzito kati ya tan o hadi tan 11 | 7,000/= |
| 4 | Kulaza gari ndani ya soko, eneo la mzani kwa siku moja | 15,000/= |

27. ADA YA MAEGESHO YA VYOMBO VYA UVUVI

| Na | AINA YA CHOMBO | ADA KWA KILA MSIMU/GIZA |
|---|---|---|
| 1 | Mitumbwi chini ya mita 11 | 20,000/= kila mtumbwi mmoja |

28. ADA YA VYOMBO VYA USAFIRISHAJI ZIWANI

| Na | AINA YA CHOMBO | KIASI CHA ADA KWA SAFARI |
|---|---|---|
| 1 | Ngama | 5,000/= |
| 2. | Mitumbwi ya injini yenye urefu zaidi ya mita 11 | 5,000/= |
| 3 | Meli za mizigo/abiria | 20,000/= |

**29. USHURU WA KITUO CHA KUOSHA VYOMBO VYA USAFIRI**

| **Na** | **Eneo kilipo kituo** | **Ushuru kwa mwezi** |
|---|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Kituo kilichopo mjini kati kata ya Kirumba, Kitangiri, Nyamanoro, Buzuruga, Mecco, Pasiansi, Nyasaka | Tshs. 50,000/= |
| 2. | Kituo kilichopo pembezoni kwenye kata nyingine | Tsh. 20,000/= |

30. USHURU WA VIWANDA VYA TOFALI

| Na. | Kiwanda cha tofali | Kiwango cha Ushuru kwa Mwezi. |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa watengenezaji wa matofali | 30,000/= |
| 2. | Ushuru wa pavements | 30,000/= |

31. USHURU WAVITUO VYA KUTENGENEZA SAMANI

| Na. | Ushuru wa kutengeza samani | Kiwango cha Ushuru kwa Mwezi. |
|---|---|---|
| 1. | Kituo cha kutengeneza samani | 30,000/= |

32. USHURU WA GEREJI

| Na. | Ushuru wa Gereji | Kiwango cha Ushuru kwa Mwezi. |
|---|---|---|
| 1. | Gereji za aina zote | 30,000/= |

33. ADA YA USAJILI WA KIKUNDI CHA KIJAMII (CBO)

| Na. | KIKUNDI | TSH. KWA KIKUNDI KWA MWAKA |
|---|---|---|
| 1 | ADA YA USAJILI | 10,000/= |

34. USHURU WA SAMAKI NA MAZAO YA ZIWANI

| NA | AINA YA ZAO | KIASI KWA KILO MOJA /LITA. (TSH) |
|---|---|---|
| 1 | Samaki wabichi | 50 |
| 2 | Samaki wakavu | 50 |
| 3 | Dagaa wakavu | 40 |
| 4 | Furu | 40 |
| 5 | Dagaa wabichi | 10 |
| 6 | Uduvi | 20 |
| 7 | Konokono | 20 |
| 8 | Mabondo mabichi | 1,700 |
| 9 | Mabondo makavu | 2,300 |
| 10 | Mazao mengineyo (vichwa vya samaki, chips, fish meal) | 20 |



Scanned with CamScanner

| | | |
|---|---|---|
| 11 | Mafuta ya samaki lita 1 | 50 |
| 12 | Mazao mengine ya ziwani | 20 |

35. ADA YA KUSAJILI TAXI ZA MTANDAO

| NA. | UJAZO WA TAX | KIASI KWA MWAKA |
|---|---|---|
| 1 | Abiria 1-5 | 50,000/= |
| 2 | Abiria 1-8 | 70,000/= |
| 3 | Abiria 1-10 | 90,000/= |

## JEDWALI LA PILI

(*Limetengenezwa chini ya aya ya 15*)

### HATI YA KUKIRI KOSA

Mimi ………………………………. nakiri mbele ya ………………………………. ambaye ni Mkurugenzi, kwamba, mnamo tarehe ……. ya mwezi ……… mwaka ………… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya Kifungu cha ………… cha Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ya mwaka 2022.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, kwa hiyari yangu niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru unaodaiwa pamoja na faini.

Nathibitisha maelezo hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa kwa hiari yangu na ufahamu wangu.

Leo tarehe …… ya mwezi …………… mwaka …………

Jina………………………..…………………………

Saini……………

MBELE YA:

JINA: ……………………………………………………

CHEO : …………………………………………………..

SAINI: …………………………………………………...



Scanned with CamScanner

Nembo ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela imebandikwa kwenye sheria ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa katika kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kilichofanyika tarehe 10/09/2022.

Eng. MODEST JOSEPH APOLINARY,
*Mkurugenzi wa*
*Halmashauri ya Manispaa*
*Ilemela*

MH. RENATUS BAHEBE MULUNGA
*Mstahiki Meya wa Halmashauri ya Manispaa*
*Ilemela*

L.S

NAKUBALI

INNOCENT L. BASHUNGWA
*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais,*
*TAMISEMI*

*Dodoma*
23/6/2022



Scanned with CamScanner

TANGAZO LA SERIKALI NA . 504 la tarehe 22/7/2022

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)

(SURA 288)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 89)*

SHERIA NDOGO ZA AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA, 2022

## SEHEMU YA KWANZA
## UTANGULIZI

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za Afya na Usafi wa Mazingira za Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela za Mwaka, 2022.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi itatumika katika eneo lote lilipo katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa Muktadha utakapo hitaji vinginevyo: -

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Umma atakayeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

"Chakula" maana yake ni kitu chochote kinacholiwa au kunywewa na binadamu isipokuwa madawa, hii ni pamoja na-

(a) kitu chochote kinachotumika katika matengenezo ya chakula;

(b) kitu chochote kinachoongeza ladha ya chakula;

(c) kitu chochote kinachobadili rangi ya chakula (binzari na vingine vinavyofanana na hivi);



Scanned with CamScanner

"Choo cha kuvuta" maana yake ni choo ambacho kimejengwa na kuunganishwa na mfumo wa maji na kuwa na tanki ya kusukuma maji kwa ajili ya kuondoa uchafu hadi mahali palipo andaliwa.

"Choo bora" maana yake ni choo chochote cha maji chenye sakafu, banda imara la kudumu, limeezekwa, lina mlango imara, bomba la kutolea hewa chafu na lenye mfuniko kwenye tundu la choo na shimo salama na safi kwa ajili ya kutupa kinyesi na mkojo wa binadamu, lililojengwa kwa vifaa vya kudumu, lenye vipimo vya futi 4 x 3 na kimo cha futi 12 na zaidi;

"Choo cha umma" maana yake ni choo kilichojengwa na Halmashauri au wakala wake kwa matumizi ya umma;

"eneo la wazi" maana yake ni eneo lililo chini ya Halmashauri ambalo limekatazwa kufanyia shughuli ambayo haihusiani na matumizi yaliyokusudiwa;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela;

"hati ya usafi" maana yake ni hati itakayotolewa na Afisa Mwidhiniwa inayothibitisha kukaguliwa kwa maeneo yote yaliyotajwa katika Sheria Ndogo hizi kulingana na Kanuni za Afya;

"Jengo la biashara" maana yake ni jengo lolote lililojengwa na kuidhinishwa na Halmashauri kufanya biashara iliyokusudiwa;

"kaya"maana yake ni familia ya watu akiwemo baba, mama, mtoto au watoto na mtu mwingine yeyote anayeishi na familia hiyo, au watu wanaokaa katika nyumba moja na kuishi kama familia au mtu yeyote anayeishi peke yake katika chumba au nyumba;

"kero au chukizo" maana yake ni kitu chochote ambacho kipo katika hali yoyote iwe kinatumika, kimewekwa, kimejengwa, au ni kichafu kiasi cha kusababishi-

(a) hatari kwa viumbe na maisha ya binadamu;

(b) harufu mbaya au harufu ya kuudhi;

(c) kuzaliana kwa wadudu na wanyama hatari kama vile inzi, mende, sisimizi, panya, nyoka, nyuki, kunguni au viumbe wengine hatari.

(d) magonjwa kwa binadamu.



Scanned with CamScanner

"kituo cha taka" maana yake ni kizimba cha kukusanya taka kilichowekwa na Halmashauri kwa madhumuni ya kuweka taka ngumu kabla ya kusafirishwa hadi dampo la taka ngumu la Halmashauri;

"maji taka"maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"mkazi" maana yake ni mtu yeyote anayeishi katika eneo la Halmashauri na ambaye ana kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Halmashauri;

"mkaguzi" maana yake ni Afisa yoyote wa Halmashauri anayesimamia utekelezaji wa Sheria ndogo hizi;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri au Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Mmiliki" maana yake ni mtu yeyote ambaye ana miliki ardhi, sehemu za starehe, nyumba za kulala wageni, nyumba za kuuzia vyakula, kumbi za starehe, mpangaji, wakala wa mpangishaji wa nyumba au jengo na makazi yoyote ndani ya eneo la Halmashauri;

"mzalishaji wa taka ngumu" maana yake ni mtu yeyote, kaya, taasisi, biashara, kiwanda ambaye katika kutekeleza shughuli zake huzalisha taka;

"Pipa la taka" maana yake ni chombo chochote chenye mfuniko kinachoweza kuhifadhi taka ngumu zinazozalishwa majumbani, sehemu za biashara, maofisini ili zisisambae na kuchafua mazingira;



Scanned with CamScanner

SEHEMU YA PILI

USAFI WA MAZINGIRA

Wajibu wa kufanya usafi wa mazingira

4. (1)Itakuwa ni wajibu wa kila mkazi au mfanyabiashara anayemiliki au anayeishi katika eneo la nyumba kuhakikisha kwamba anafanya usafi wa mazingira yanayozunguka makazi au eneo lake kwa kuhakikisha kwamba;

(a) majani yanayozunguka nyumba yake yanakatwa au kupaliliwa katika eneo lote hadi mwanzo wa mipaka ya barabara ya mbele ya nyumba yake au eneo lake;

"Taka"maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"Takangumu"maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"taka za majumbani" maana yake ni mabaki ya chakula, maganda ya matunda, majivu, kinyesi cha mifugo, taka za bustani, marapurapu ya nguo, karatasi za aina mbalimbali na vitu vingine ambavyo baada ya kuvitumia hutupwa;

"Taka za viwandani" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"Uchafu hatari" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Mazingira;

"Uchunguzi wa afya" maana yake ni hali ya mtu kupima afya yake kwa kuchukuliwa vipimo vya ndani na nje ya mwili ili kubaini kuwepo kwa vijidudu vya magonjwa vinavyoweza kuleta maambukizi;

"Ufugaji wa ndani" maana yake ni ufugaji wa mifugo ndani ya nyumba, banda au zizi ndani ya eneo lililoruhusiwa na Halmashauri; na

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi au kikundi cha watu, kampuni, taasisi au shirika lililoteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;



Scanned with CamScanner

(b) takataka ngumu na laini ikiwa ni pamoja na mifuko ya plastiki zitakusanywa, kuhifadhiwa nakupelekwa katika eneo lililoruhusiwa na Halmashauri; na

(c) kila mmiliki wa nyumba au kiwanja au eneo lolote ambalo halijaendelezwa anawajibika kufanya usafi katika eneo hilo mara kwa mara.

Usafi wa mifereji ya maji ya mvua.

5. Ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba kuondoa uchafu kama vile, mchanga, majani, nyasi au vitu vingine vinavyofanana na hivyo kwenye mfereji wa maji ya mvua unaozunguka au kupita kando ya nyumba yake au eneo la biashara yake, kiwanja chake na kuhakikisha mfereji huo unakuwa safi wakati wote.

Wajibu wa kupanda miti

6. (1) Ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba au eneo kuhakikisha anapanda miti 2 katika nyumba yake au eneo analomiliki.

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kukata miti bila kibali kutoka kwa Afisa mwidhiniwa

Usafi wa siku

7. Kila siku itakuwa ni siku maalum ya ukaguzi wa jumla wa Usafi wa Mazingira ambapo wakaguzi kutoka Halmashauri watapita kufanya ukaguzi wa mazingira na itakapobainika kuwa mtu yeyote hajafanya usafi au kuna uchafuzi wowote katika eneo husika, hatua stahiki zitachkuliwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Usafi wa kila jumamosi

8 Kila Jumamosi ya mwisho ya kila mwezi utafanyika usafi wa mazingira wa jumla kuanzia saa 1:00 asubuhi hadi saa 4:00 asubuhi, ambapo kila mtu au taasisi itawajibika kushiriki katika zoezi la usafi wa mazingira na wakati wote wa muda wa usafi wa mazingira shughuli zote zitasimamishwa isipokuwa huduma muhimu kama zitakavyoainishwa na Halmashauri.



Scanned with CamScanner

Kupaka rangi majengo

9. Halmashauri itahamasisha wamiliki wa nyumba au wapangaji au wafanyabiashara kupaka rangi nyumba au duka ndani na nje pindi linapochakaa.

Wajibu wa kuondoa na kudhibiti mazalia ya mbu.

10. Ni wajibu wa mmiliki wa nyumba kuhakikisha kuwa hakuna madimbwi ya maji, maji machafu, takataka au kitu chochote cha majimaji au kigumu ambacho kinaweza kuruhusu kuwepo wa mazalia ya mbu au wadudu wengine wenye madhara kwa afya ya binadamu.

Biashara ya miwa na matunda

11. Itakuwa ni wajibu wa kila mfanyabiashara ya matunda au miwa kuhakikisha kuwa ana chombo maalum cha kuhifadhia maganda au mabaki ya matunda.

Upulizaji dawa

12. Ni marufuku kwa mtu yeyote kuendesha biashara ya upuliziaji dawa au biashara ya kuuwa wadudu katika nyumba yoyote au mahali popote bila kuwa na cheti cha taaluma kinacho tambuliwa na Serikali na awe na leseni hai kutoka Halmashauri.

Matengenezo ya magari, pikipiki, mitambo na kuegesha magari mabovu

13. (1) Hakuna mtu au taasisi itakayoruhusiwa kufanya matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo isipokuwa kwenye karakana, gereji au maeneo yaliyoruhusiwa na Halmashauri.

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuegesha gari bovu kwenye njia ya waenda kwa miguu, mtaa, uchochoro, mtaro, maeneo ya wazi, barabarani na kusababisha adha kwa wakazi au watumiaji wa njia hiyo.

Scanned with CamScanner

SEHEMU YA TATU
UIMARISHAJI WA AFYA

Usalama wa maji ya kunywa. 14. Ni wajibu wa kila mkazi kuhakikisha kwamba maji yote yanayotumika kwa kunywa ni safi na salama kwa kuyachemsha bila kujali yametoka kwenye chanzo gani cha maji.

Utengenezaji, na uuzaji vyakula. 15. Ni marufuku kwa mtu yeyote kutengeneza, kuchoma, kupika, kuchemsha au kuuza chakula cha aina yoyote mahali popote mtaani, uchochoroni, magengeni au kwenye nyumba yoyote mpaka awe ametimiza masharti na kanuni za afya na amepata kibali kutoka kwa Afisa Afya wa Halmashauri.

Uuzaji vyakula vilivyopikwa. 16. Ni wajibu wa kila mtu anayeendesha biashara ya vyakula vya kupikwa au kukaangwa kuhakikisha kwamba vyakula hivyo vinahifadhiwa kwenye sanduku lililotengenezwa kwa mbao safi na kuwekwa kioo kuzuia inzi, vumbi na wadudu waletao madhara kwa afya ya binadamu.

Usalama wa vyakula. 17. Ni marufuku kwa mtu yeyote kuuza vyakula visivyopikwa vikiwa vimewekwa chini, vyakula vyote vitatakiwa kuwekwa juu ya meza.

Uzuiaji wa shughuli mbalimbali wakati wa magonjwa ya mlipuko 18. Afisa mwidhiniwa anaweza kutoa amri ya kuzuia shughuli yoyote isifanyike kama vile utengenezaji wa vyakula, pombe, mijumuiko, sherehe na mikusanyiko yoyote kwa kutangaza kwa njia ya kipaza sauti, maandishi au kupitia vyombo vya habari endapo atakuwa na sababu ya kuamini kwamba shughuli hiyo inaweza kusababisha kuenea kwa magonjwa ya mlipuko na kuleta athari kwa maisha ya binadamu.



Scanned with CamScanner

Ukamataji wa vyombo vilivyotumika kuhifadhia chakula

19. (1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kukamata vyakula, vyombo au vifaa vingine vyovyote vitakavyokuwa vinatumika mara baada ya kutolewa amri ya zuio la kufanyika kwa shughuli ya uuzaji wa vyakula wakati wa magonjwa ya mlipuko.

(2) Endapo vyakula vitakavyo kamatwa vitakuwa ni vile ambavyo vinaweza kuharibika kwa haraka Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuviharibu kwa kujaza fomu ya kuharibu ambayo sharti ithibitishwe na Mahakama.

(3) Endapo vyakula vilivyokamatwa vitakuwa haviharibiki kwa haraka Halmashauri itakuwa na jukumu la kuvihifadhi hadi mwisho wa amri ya zuio.

(4) Halmashauri haitahusika na gharama zozote zitakazotokea endapo vyombo vitaharibika, isipokuwa kama uharibifu huo utakuwa umesababishwa kwa uzembe wa Afisa wa Halmashauri.

Machinjio na madukaya nyama

20. (1) Ni wajibu wa kila mmiliki wa duka la kuuzia nyama kuhakikisha kwamba duka lake-

(a) ni jengo la kudumu lililosakafiwa kwa marumaru nyeupe hadi urefu wa futi 6 kutoka usawa wa sakafu;
(b) lina maji safi, na misumeno ya kukatia nyama;
(c) lina kabati ya vioo na jokofu la kuhifadhia nyama na sehemu za mizani;
(d) lina pipa la kuhifadhia taka taka;.
(e) muuzaji ana vazi jeupe pamoja na aproni nyeupe; na
(f) muuzaji anapima afya kila baada ya miezi sita

Kuchinja na kuuza nyama mahali pasiporuhusiwa

21. Ni kosa kwa mtu yeyote kuchinja au kuuza nyama ya aina yoyote katika maeneo yasiyo ruhusiwa na Halmashauri.



Scanned with CamScanner

Uendeshaji wa biashara ya nyumba za kulala wageni na hosteli

22. (1) Ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba za kulala wageni na hosteli au nyumba za biashara kuhakikisha anapata kibali kutoka Halmashauri kabla hajaanza biashara.

(2) Endapo mmiliki hatakidhi masharti ya kiafya Halmashauri inaweza kuzuia kibali cha kuendesha biashara ya nyumba ya kulala wageni au hosteli mpaka hapo mmiliki atakapokuwa amekidhi masharti yaliyotolewa na Halmashauri.

Mahitaji ya nyumba ya wageni na Hosteli

23. Kibali cha kuendesha biashara ya nyumba ya kulala wageni, mgahawa, hoteli na hosteli kitatolewa baada ya Halmashauri kujiridhisha kuwa katika majengo hayo kuna-

(a) mwanga na hewa ya kutosha;
(b) nafasi na vifaa (samani ) za kutosha;
(c) uimara wa jengo;
(d) mfumo wa uondoshaji wa maji taka na taka ngumu wa kuaminika;
(e) usafi wa jumla wa jengo na vifaa vyake;
(f) vyoo na mabafu kwa jinsia zote;
(g) vifaa vya zima moto;
(h) tanki la kuhifadhia maji safi; na
(i) vyoo na bafu vilivyosakafiwa kwa vigae au marumaru na kuta zake zimewekwa vigae kiasi cha futi 6 kutoka usawa wa sakafu.

Upimaji wa afya

24. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila Mmiliki wa hoteli, wafanyakazi wa machinjio, mgahawa, baa, bucha, sehemu za kuokea mikate, nyumba za kulala wageni, grosari kupima afya kila baada ya miezi sita na watalipa ada ya upimaji wa afya kiasi cha shilingi elfu kumi.

(2) Mtu yeyote anayetengeneza chakula kwa ajili ya kuuza atalazimika kupima afya kila baada ya miezi sita na atalipa ada ya upimaji wa afya kiasi cha shilingi elfu kumi.



Scanned with CamScanner

(3) Mmiliki yeyote atakayeruhusu mhudumu wake kufanya kazi bila kupimwa afya yake atakuwa ametenda kosa chini ya sheria ndogo hizi.

Uwezo wa kukagua

25. Afisa mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia katika jengo lolote wakati wowote au chombo chochote kukagua utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

Kufungwa kwa jengo la biashara lisilokidhi masharti ya afya

26. Afisa mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kutoa Ilani ya kufunga kwa biashara yoyote au jengo ambalo halijakaguliwa au lililokaguliwa na kukutwa limekiuka kanuni na masharti ya afya.

Ada ya ukaguzi wa afya

27. Halmashauri itatoza ada ya ukaguzi wa afya ambayo italipwa kwa mwaka kabla ya mwombaji kupewa leseni ya biashara ambayo viwango vyake vitakuwa kama vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

Muda wa kulipa ada

28. (1) Ada ya ukaguzi wa afya italipwa kila mwanzo wa mwaka wa fedha wa Halmashauri yaani mwezi Julai.

(2) Mtu yeyote atakayeshindwa kulipa ada katika kipindi cha miezi miwili baada ya mwaka wa fedha kuanza atawajibika kulipa kiwango hicho pamoja na adhabu ya asilimia hamsini ya kiwango anachodaiwa.

## SEHEMU YA NNE
## UZOAJI TAKA

Taka kutupwa kwenye gari la taka

30. Kila kaya au wapangaji katika nyumba au wafanyabiashara watakuwa na jukumu la kutunza, kubeba na kupeleka taka walizozizalisha na kuzitupa moja kwa moja kwenye gari la kubeba taka kwa kuzingatia ratiba na utaratibu uliowekwa na Halmashauri au kuzitupa katika makasha ya taka yaliyowekwa katika baadhi ya maeneo.



Scanned with CamScanner

Jukumu la kuwa na chombo cha kuhifadhia taka

31. Kila mwenye nyumba au mpangaji, mmiliki au msimamizi wa eneo la biashara, taasisi na ofisi ndani ya Halmashauri anatakiwa awe na pipa dogo au ndoo au chombo au kifaa chochote chenye mfuniko yaani "waste bins"kwa ajili ya kuhifadhia taka zinazozalishwa katika eneo hilo kwa ajili ya madhumuni yaliyotajwa.

Wajibu wa mmiliki wa chombo cha usafiri

32. (1) Mmiliki au dereva wa chombo cha usafiri wa umma anawajibika kuweka chombo au kifaa cha kuhifadhia taka ndani ya gari kwa ajili ya abiria wake.

(2) Kila mmiliki au dereva wa chombo cha kusafirishia mizigo, taka au madini ya ujenzi atatakiwa kuhakikisha anaweka vifaa vya kufunika bidhaa anazosafirisha ili kutoruhusu bidhaa hizo kudondoka au kumwagika na kuchafua mazingira.

Marufuku kutupa taka hovyo

33. 1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kutupa takataka ngumu au laini mahali popote pasipo ruhusiwa rasmi kwa ajili ya kutupa takataka za aina hiyo.

Ada ya uzoaji taka

34. (1 ) Halmashauri imeutenga mji katika kanda tatu za ukusanyaji, uzoaji na utupaji wa taka ngumu: KANDA A- Nyamanoro, Kirumba, Buzuruga, Mecco, Pasiansi, Nyasaka, Kitangiri.KANDA B- Buswelu, Nyakato, Kiseke, Kawekamo, Ibungilo. KANDA C- Nyamhongolo Ilemela, Sangabuye, Bugogwa, Kayenze, Kahama, Shibula. Kwa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la sheria Ndogo hizi.

Scanned with CamScanner

(2 ) Halmashauri itatoza gharama za uzoaji na utupaji wa taka katika dampo la Halmashauri kutoka kwa mawakala, wamiliki wa taasisi mbalimbali, viwanda na makampuni pamoja na wazalishaji wengine wa taka kwa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hizi.

(3 )Ada ya kila mwezi italipwa kila tarehe 30 ya kila mwezi ndani ya mwezi husika, isipokuwa kwa aina ya biashara itakayotozwa kwa siku, na italipwa kwa Afisa mwidhiniwa ambaye atatoa stakabadhi ya malipo ya kielektroniki yatakayolipwa na atajaza katika rejista ya wazalishaji taka.

(4) Halmashauri haitotoza ada ya uzoaji taka ngumu kutoka kwenye kaya maskini ambazo zimejiunga kwenye mfuko unaohudumia kaya zenye kipato cha chini sana au masikini kabisa TASAF au mfuko mwingine wowote unaotambulika kisheria kutoa huduma hizo. Pia Wakala, Mtu binafsi, Kampuni au kikundi cha kijamii hakitaruhiswa kutoza ada ya usafi kutoka kaya zote zilizounganishwa kwenye mifuko inayohudumia kaya masikini.

(5)Iwapo mzalishaji wa taka atashindwa kulipia gharama ya huduma ya uzoaji taka kwa kipindi cha miezi miwili mfululizo Halmashauri itamchukulia hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani.

Uanzishwaji wa vikundi jamii

35. (1)Halmashauri itakuwa na jukumu la kuhamasisha uundaji wa Vikundi vya kijamii, kampuni, wakala, au mtu binafsi na kuwataka kufanya shughuli za udhibiti wa taka ngumu pamoja na usafi wa mazingira baada ya kuingia mkataba na Halmashauri.

(2)Majukumu mahsusi ya wakala, kikundi, kampuni au mtu binafsi yatakuwa kama ifuatavyo;-

(a) kukusanya, kuzoa na kusafirisha taka kutoka maeneo yote ya uzalishaji na kuzipeleka katika dampo kuu la buhongwa; na

(b) kukusanya ada ya usafishaji na uondoshaji taka katika maeneo ya makazi na biashara na kuwasilisha kiasi chote asilimia mia moja 100% kilichokusanywa kwenye akaunti ya Halmashauri ambapo Halmashauri itarudisha



Scanned with CamScanner

kwa msafishaji asilimia 70% ya makusanyo yote na kiasi cha asilimia thelathini 30% kitabaki Halmashauri kama mapato ya ndani.

Wajibu wa kuwa na pipa la taka

36. Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba au mpangaji au mfanyabiashara kuhakikisha kuwa ana chombo imara chenye mfuniko kwa ajili kuhifadhia taka ngumu kabla hazijachukuliwa na Halmashauri kwa ajili ya kwenda kutupwa.

Kutupa taka katika sehemu maalum

37. Itakuwa ni wajibu wa kila mkazi kuhakikisha kwamba anatupa uchafu au taka katika vyombo maalum vilivyowekwa kwa ajili ya kutunzia taka katika maeneo maalum yaliyotengwa.

Kutiririsha maji taka

39. Ni marufuku kutiririsha au kuelekeza maji kutoka vyooni, bafuni, karoni, baada ya kufua au kuosha vyombo kwenda sehemu yoyote isiyotengwa kuhifadhi maji taka.

Taka za viwanda

40. (1) Itakuwa ni marufuku kwa kiwanda chochote kutoa au kusababisha kutoa uchafu wa aina yoyote, maji machafu au harufu mbaya na kusababisha kero kwa wakazi wa eneo la Halmashauri.

(2) Ni wajibu wa kila mwenye kiwanda kuhakikisha kuwa taka kama vile vumbi, maganda, moshi na takataka nyingine zinazoweza kuleta kero au adha kwa ujumla haziwafikii wala hazileti madhara kwa binadamu na viumbe wengine hai.

Uteuzi wa wakala

41. Halmashauri inaweza kuteua wakala, kikundi cha jamii au mtu binafsi kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.



Scanned with CamScanner

## SEHEMU YA TANO
## UJENZI NA MATUMIZI YA VYOO

Wajibu wa kuwa na choo na kukitumia

42. Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba au mpangaji kuhakikisha kwamba nyumba yake ina choo safi, imara na madhubuti kwa matumizi ya wakazi wa nyumba hiyo na kuhakikisha kinatumika wakati wote.

Umbali wa kujenga choo

43. Choo kinatakiwa kijengwe umbali wa zaidi ya mita sitini (60) kutoka kisima au chanzo chochote cha maji kinachotumika kwa matumizi ya nyumbani.

Vyoo vya umma

44. (1) Halmashauri inaweza kumruhusu mtu binafsi, vikundi vya watu au Taasisi kujenga vyoo vya umma katika maeneo ambayo Halmashauri itaona inafaa kufanya hivyo.

(2) Vyoo hivyo vitamilikiwa na Halmashauri au kwa ubia na wajenzi na vitakuwa ni vya kulipia kama itakavyokuwa imeelekezwa na Halmashauri katika mkataba wake na mawalaka watakaopewa kusimamia vyoo hivyo.

Vyoo vya muda katika mikusanyiko

45. Itakuwa ni wajibu wa mtu, kikundi, Taasisi yenye lengo la kukutanisha watu kwa madhumuni ya ujenzi, sherehe au sehemu yoyote ambayo itakutanisha watu kwa muda maalum endapo eneo hilo hakuna choo cha kudumu kujenga vyoo kwa matumizi ya wakati huo kwa idhini na usimamizi wa Halmashauri.

Vyoo katika majengo ya biashara

46. Kila mmiliki wa jengo la biashara atatakiwa kujenga vyoo viwili vyenye viwango vinavyokubalika chini ya Sheria Ndogo hizi kwa ajili ya matumizi ya wateja wake wa jinsia zote.



Scanned with CamScanner

Ilani ya kujenga choo

**47.** Endapo katika ukaguzi wa afya itagundulika kuwa nyumba yoyote haina choo, choo kilichopo kimejaa au hakifai kwa matumizi ya binadamu, Afisa mwidhiniwa atatoa ilani ya siku thelathini kwa mmiliki wa nyumba au mpangaji akiainisha masharti ya kurekebisha hali hiyo kama ilivyoainishwa katika Jedwali la nne la Sheria Ndogo hizi.

Ilani ya kuondoa adha au usumbufu

**48.** (1) Endapo Afisa mwidhiniwa atagundua kuwa eneo alilokagua lina adha yoyote atatoa ilani ya masaa arobaini na nane (48) kwa mmiliki wa nyumba, mpangaji, mtumiaji au mtu yeyote anayehusika akimtaka kuondoa adha hiyo kama ilivyoainishwa katika Jedwali la tano la Sheria Ndogo hizi.

(2) Mtu yeyote atakayekaidi au kushindwa kutekeleza masharti ya ilani aliyopewa ndani ya muda ulioainishwa kwenye ilani atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi.

Halmashauri kuteua mkaguzi

**49.** Halmashauri inaweza kumteua mtu yeyote kuwa mkaguzi kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa usafi katika eneo la Halmashauri.

Uwezo wa kutoa adhabu ya papo kwa papo

**50.** Chini ya Sheria Ndogo hizi mkaguzi atakuwa na uwezo wa kutoa adhabu ya papo kwa papo kwa mtu yeyote atakayekutwa amechafua mazingira kwa kutupa takataka mahali popote pasiporuhusiwa ilimradi kuwa adhabu hiyo izingatie masharti ya Sheria Ndogo hizi.

Makosa

**51.** Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo-

(a) atamzuia au kujaribu kumzuia Afisa mwidhiniwa kutekeleza wajibu wake chini ya Sheria Ndogo hizi;

(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kumzuia Afisa mwidhiniwa asitekeleze wajibu wake chini ya Sheria Ndogo hizi;



Scanned with CamScanner

(c) atamwaga takataka barabarani au katika mtaro wa maji ya mvua au uchochoroni au mahali popote hadharani au katika eneo lolote lisiloruhusiwa;

(d) ataendesha biashara ya pombe ndani ya nyumba ya makazi;

(e) atatiririsha maji machafu barabarani au katika eneo la nyumba ya jirani;

(f) ataosha magari au kufua au kunywesha mifugo na kukoroga dawa za mimea ndani ya mito, mabwawa, lambo au ndani ya chanzo cha maji au kisima kinachotumika kwa matumizi ya binadamu;

(g) atauza vyakula vilivyopikwa barabarani au nje ya majengo bila kibali;

(h) atafanya matengenezo ya magari au pikipiki au mitambo au kuendesha shughuli za viwanda katika maeneo ya wazi, makazi, barabarani, uchochoroni, au katika maeneo yasiyotengwa kwa shughuli hizo bila kuzingatia taratibu za mipango miji;

(i) ataanzisha au kufungua karakana katika majengo au majumba ya makazi au maeneo yasiyoruhusiwa;

(j) ataenda haja ndogo au kubwa hovyo barabarani, uchochoroni au upenuni au mahali popote ambapo siyo chooni;

(k) atashindwa kuhifadhi chakula kwenye kabati safi lililofunikwa na lenye kioo;

(l) atatiririsha maji safi kihorera.

Adhabu 52. Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na iwapo atapatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu au kutumikia kifungo



Scanned with CamScanner

kisichozidi miezi kumi na mbili (12) au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufililisha kosa 53. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini isiyozidi shilingi laki mbili iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari yake mwenyewe kwa maandishi na kukubali kutekeleza wajibu wake pamoja na kulipa faini anayodaiwa kama ilivyoelekezwa katika Jedwali la sita la Sheria Ndogo hizi.

Kufuta TS Na. 364 la Mwaka 2014 54. Sheria Ndogo hizi zinafuta Sheria Ndogo za (Afya na Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, 2014



Scanned with CamScanner

## JEDWALI LA KWANZA

*(limetengenezwa chini ya aya ya 27)*

### ADA YA UKAGUZI WA AFYA

| Na. | Aina ya biashara | Ada kwa mwaka |
|---|---|---|
| 1. | Baa na maduka ya vinywaji (Groceries) | 50,000/= |
| 2. | Migahawa /mama lishe | 10,000/= |
| 3. | Nyumba za wageni (Guest House) na Hoteli | 50,000/= |
| 4. | Kumbi za starehe au mikutano | 10,000/= |
| 5. | Hotel | 100,000/= |
| 6 | Kiwanda | 100,000/= |
| 5. | Majengo mengine ya biashara | 10,000/= |
| 6 | Viwanda vya matofari | 50,000/= |
| 7 | Ukaguzi wa dharura | 20,000/= |

## JEDWALI LA PILI

*(Limetengezwa chini ya aya ya 34(1))*

### ADA ZA UZOAJI TAKA NGUMU

| Na. | AINA YA BIASHARA | KANDA 'A' | KANDA 'B' | KANDA 'C' |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Kaya | 3,000/= | 3,000/= | 3,000/= |
| 2 | Tea room | 5000/= | 5000/= | 5000/= |
| 3 | Café | 9000/= | 6,000/= | 5000/= |
| 4 | Ice cream/barafu | 10,000/= | 8,000/= | 5000/= |
| 5 | Restaurant | 20,000/= | 20,000/= | 20,000/= |
| 6 | Nyumba za Wageni | 20,000/= | 16,000/= | 10,000/= |
| 7 | Dispensary (normal refuse) | 20,000/= | 16,000/= | 12,000/= |
| 8 | Health centre (normal refuse) | 24,000/= | 20,000/= | 16,000/= |
| 9 | Viwanda vidogo/garage | 10,000/= | 8,000/= | 6,000/= |
| 10 | Hotel: Vyumba 1-10 | 40,000/= | 40,000/= | 40,000/= |



Scanned with CamScanner

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | • Vyumba 11-20 | 60,000/= | 60,000/= | 60,000/= |
| | • Vyumba 21-30 | 80,000/= | 80,000/= | 80,000/= |
| | • Vyumba 31-40 | 90,000/= | 90,000/= | 90,000/= |
| | • Vyumba 41-50 | 120,000/= | 120,000/= | 120,000/= |
| | • Vyumba 61-70 | 160,000/= | 160,000/= | 160,000/= |
| | • Vyumba 71-80 | 180,000/= | 180,000/= | 180,000/= |
| | • Vyumba 81- 100 | 200,000/= | 200,000/= | 200,000/= |
| 11 | Maduka ya dawa muhimu | 20,000/= | 20,000/= | 20,000/= |
| 12 | Bucha | 16,000/= | 10,000/= | 10,000/= |
| 13 | Masoko kwa chumba (stals) | 10,000/= | 6,000/= | 4,000/= |
| 14 | Magenge | 4,000/= | 4,000/= | 4000/= |
| 15 | Wauza vyakula mitaani/sokoni | 300/= kwa siku | 300/= kwa siku | 300/= kwa siku |
| 16 | Wafanyabiashara wadogo wanaohamahama magulio | 300/= kwa siku | 300/= kwa siku | 300/= kwa siku |
| 17 | Magari ya mizigo (cargo) | 40,000/= | 40,000/= | 40,000/= |
| 18 | Biashara ndogondogo | 2000/= | 2000/= | 2000/= |
| 19 | Dobi | 2,000/= | 2,000/= | 2,000/= |
| 20 | Saloon/vinyozi | 10,000/= | 8,000/= | 6,000/= |
| 21 | Vituo vya mafuta | 40,000/= | 40,000/= | 40,000/= |
| 22 | Wauza mikaa | 6,000/= | 6,000/= | 6,000/= |
| 23 | Maduka ya jumla | 30,000/= | 20,000/= | 16,000/= |
| 24 | Maduka ya vyakula (super markets) | 40,000/= | 40,000/= | 40,000/= |
| 25 | Maduka ya Hardware | 50,000/= | 40,000/= | 20,000/= |
| 26 | Maduka ya rejareja | 20,000/= | 16,000/= | 10,000/= |
| 27 | Dry cleaner | 20,000/= | 20,000/= | 10,000/= |
| 28 | Radio service | 10,000/= | 8,000/= | 4,000/= |
| 29 | Sonara (g/smith) | 8,000/= | 6,000/= | 6,000/= |
| 30 | Laboratories | 16,000/= | 14,000/= | 10,000/= |
| 31 | Furniture/carpentry | 20,000/= | 10,000/= | 10,000/= |
| 32 | Video show | 10,000/= | 8,000/= | 6,000/= |
| 33 | Battery charge | 6,000/= | 6,000/= | 4,000/= |
| 34 | Refrigerate services | 6,000/= | 6,000/= | 6,000/= |
| 35 | Welding | 6,000/= | 6,000/= | 4,000/= |
| 36 | Plumbers | 8,000/= | 6,000/= | 4,000/= |
| 37 | Kuuza mapipa | 6,000/= | 6,000/= | 4,000/= |
| 38 | Scale services | 4,000/= | 4,000/= | 4,000/= |
| 39 | Posho mills | 40,000/= | 30,000/= | 20,000/= |
| 40 | Pombe shop | 10,000/= | 6,000/= | 4,000/= |
| 41 | Garments | 16,000/= | 12,000/= | 10,000/= |
| 42 | Wachoraji | 4,000/= | 4,000/= | 4,000/= |
| 43 | Soda (whole scale) | 30,000/= | 20,000/= | 16,000/= |



Scanned with CamScanner

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 44 | Studio | 8,000/= | 8,000/= | 8,000/= |
| 45 | Spare parts | 16,000/= | 10,000/= | 6,000/= |
| 46 | Mafuta ya taa mitaani | 2,000/= | 2,000/= | 2,000/= |
| 47 | Karakana | 20,000/= | 20,000/= | 20,000/= |
| 48 | Bakeries | 20,000/= | 20,000/= | 20,000/= |
| 49 | Kuuza magazeti | 2,000/= | 2,000/= | 2,000/= |
| 50 | Computer services | 10,000/= | 6,000/= | 4,000/= |
| 51 | Godowns | 16,000/= | 10,000/= | 10,000/= |
| 52 | Stores | 10,000/= | 6,000/= | 4,000/= |
| 53 | Water kiosks | 2,000/= | 2,000/= | 2,000/= |
| 54 | Fish maws | 5,000/= | 5,000/= | 5,000/= |
| 55 | Mabasi ya express | 4,000/= | 4,000/= | 4,000/= |
| 56 | Night club | 40,000/= | 30,000/= | 20,000/= |
| 57 | Makanisa | 10,000/= | 10,000/= | 10,000/= |
| 58 | Misikiti | 10,000/= | 10,000/= | 10,000/= |
| 59 | Maduka makubwa ya dawa(Pharmacy) | 40,000/= | 40,000/= | 40,000/= |
| 60 | Grocery | 20,000/= | 16,000/= | 12,000/= |
| 61 | Baa | 30,000/= | 20,000/= | 16,000/= |
| 62 | Waosha magari | 20,000/= | 16,000/= | 12,000/= |
| 63 | Wauza kuku Sokoni | 5000/= | 5000/= | 5000/= |
| 64 | Shule za msingi | 10,000/= | 10,000/= | 10,000/= |
| 65 | Shule za sekondari | 20,000/= | 20,000/= | 20,000/= |
| 66 | Taasisi za dini | 10,000/= | 10,000/= | 10,000/= |
| 67 | Viwanda (taka nzito kwa tani) | 10,000/= | 10,000/= | 10,000/= |
| 68 | Viwanda (taka nyepesi kwa trip) | 40,000/= | 40,000/= | 40,000/= |
| 69 | Hospitali | | | |
| | Vitanda 1-10 | 20,000/= | 20,000/= | 20,000/= |
| | Vitanda 11-20 | 24,000/= | 24,000/= | 24,000/= |
| | Vitanda 21-30 | 30,000/= | 30,000/= | 30,000/= |
| | Vitanda 31-40 | 40,000/= | 40,000/= | 40,000/= |
| | Vitanda 41-50 | 50,000/= | 50,000/= | 50,000/= |
| | Vitanda 61-70 | 60,000/= | 60,000/= | 60,000/= |
| | Vitanda 71-80 | 80,000/= | 80,000/= | 80,000/= |
| | Vitanda 81-90 | 120,000/= | 120,000/= | 120,000/= |
| | Vitanda 91-100 | 160,000/= | 160,000/= | 160,000/= |
| | Vitanda 101 na kuendelea | 200,000/= | 200,000/= | 200,000/= |

## ADA YA UNYONYAJI MAJITAKA

| SN | AINA YA HUDUMA | KIASI KWA SAFARI MOJA (trip) |
|---|---|---|
| 1 | Nyumba ya kuishi | 100,000/= |
| 2 | Taasisi | 120,000/= |
| 3 | Viwanda | 150,000/= |
| 4 | Kukodi gari nje ya Manispaa | 500,000.00 kwa siku bila gharama za mafuta |



Scanned with CamScanner

ADA YA KUPULIZIA WADUDU

(i) Ada ya kupulizia dawa ya wadudu (Fumigation) ambayo itafanywa na Halmashauri shs. 5000/- kwa mita za mraba za eneo (per square meter)
(ii) Ada ya usimamizi wa kunyunyizia dawa ya wadudu unaofanywa na watu binafsi shs. 50,000/- kwa kazi.

---

JEDWALI LA TATU

---

(Limetengenezwa chini ya aya ya 34 (2)

ADA YA UTUPAJI TAKA KATIKA DAMPO LA HALMASHAURI.

| SN | AINA YA CHOMBO | KIASI KWA KILA SAFARI / TRIPU. |
|---|---|---|
| 1. | Bajaji | 3000/= |
| 2 | Gari ndogo tani 1 hadi tani 3.9 | 5000/= |
| 3 | Gari tani 4 hadi na kuendelea | 10,000/= |

---

JEDWALI LA NNE

---

*(Limetengezwa chini ya aya 47)*

ILANI YA KUJENGA CHOO

**Ilani hii imetolewa kwa mujibu wa kifungu cha (45) cha Sheria Ndogo ya (Afya na Usafi wa Mazingira) ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, 2022.**

**SEHEMU 'A'**
**Ndugu.......................wa Mtaa/Kijiji......................Kata ya.....................**
**Unaarifiwa kwamba katika ukaguzi uliofanyika**
**Tarehe......mwezi...........mwaka..............**



Scanned with CamScanner

Katika nyumba yako ya Biashara/kuishi/kutolea Huduma*/ Namba............
iliyopo eneo la ..................katika Kitongoji/Mtaa*..........Kijiji
cha..............Kata ya.............
Imekuwa haina choo/ choo kimejaa/kimeharibika* hivyo unaamriwa kutekeleza mambo yafuatayo;

(1) ..........................................................................................
......

(2) ..........................................................................................
......

(3) ..........................................................................................
......

(4) ..........................................................................................
......

SEHEMU 'B'
Unapewa muda wa siku thelathini (30) tu tangu siku ya kupokea ilani hii kutekeleza maelekezo yote yaliyoelezwa katika sehemu 'A' ya Ilani hii,

SEHEMU 'C'
Ukaguzi wa kuthibitisha utekelezaji wa maelekezo uliyopewa utafanyika tarehe..................endepo utashindwa kutekeleza maelekezo ndani ya muda uliopewa Halmashauri itakuchukulia hatua kali za kisheria bila kukupa taarifa nyingine.

.......................................
AFISA MWIDHINIWA

IMETOLEWA NA;
Jina;............................
Saini...........................
Wadhifa.......................

*Futa lisilotakiwa

## JEDWALI LA TANO

*(Limetengezwa chini ya aya 48)*

## ILANI YA KUONDOA KERO

Ilani hii imetolewa kwa mujibu wa Kifungu cha 48 cha Sheria Ndogo ya (Afya na Usafi wa Mazingira) ya Halmashauri ya manispaa ya ilemela za mwaka 2022.

SEHEMU 'A'

Ndugu…………………..........wa Mtaa/Kijiji……………Kata ya………………… Unaarifiwa kwamba katika ukaguzi uliofanyika

Tarehe……mwezi………..mwaka….

Katika nyumba yako ya Biashara/kuishi/kutolea Huduma/kiwanja* iliyopo eneo la…………………………………………………………………………………

kumekutwa machukizo/kero/uchafu*; kama ifuatavyo;

1) …………………………………………………………………………
2) …………………………………………………………………………
3) …………………………………………………………………………
4) …………………………………………………………………………

SEHEMU 'B'

Kwa ilani hii unaamriwa kurekebisha/kuondoa/kusafisha* kwa;

1. …………………………………………………………………………
2. …………………………………………………………………………
3. …………………………………………………………………………
4. …………………………………………………………………………

SEHEMU 'C'

Unapewa muda wa masaa arobaini na nane (48) tangu siku ya kupokea ilani hii, unatakiwa kutekeleza yote yaliyoelezwa katika sehemu 'B' ya Ilani hii, kushindwa kwako kutekeleza ndani ya muda uliopewa Halmashauri italazimika kukuchukulia hatua kali za kisheria bila kulazimika kukupa taarifa nyingine.



Scanned with CamScanner

....................................
AFISA MWIDHINIWA

IMETOLEWA NA;
Jina:...................................
Saini:.......................................
Tarehe:.......................................

IMEPOKELEWA NA;
Jina;............................
saini.......................................
Wadhifa.........................

*Futa lisilohusika



Scanned with CamScanner

JEDWALI LA SITA

(*Limetengezwa chini ya aya* 53)

SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA (USAFI WA MAZINGIRA) ZA MWAKA 2022.

HATI YA KUKIRI KOSA

Mimi...............................................................Nakiri mbele ya................................................Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kwamba mnamo tarehe......... ya mwezi wa.....................mwaka.......... nilikutwa na kosa kwa kukiuka masharti ya aya .................. ya Sheria Ndogo ya (Usafi wa Mazingira) ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela za mwaka 2022, na nipo tayari kulipa kiasi cha faini ninachodaiwa kama kifungu cha 53 kinavyoeleza.

Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Tarehe..................................Sahihi...........................



Scanned with CamScanner

Nembo ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela imebandikwa kwenye sheria ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa katika kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kilichofanyika tarehe 10/9/2022.

ENG. MODEST JOSEPH APOLINARY,
*Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa Ilemela*

MH. RENATUS BAHEBE MULUNGA
*Mstahiki Meya wa Halmashauri ya Manispaa Ilemela*

L.S

NAKUBALI

INNOCENT L. BASHUNGWA
*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI*

*Dodoma*
23/6/2022



Scanned with CamScanner

TANGAZO LA SERIKALI NA . 505 la tarehe 22/7/2022

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya aya ya 6(1) (u) na 16 (1))*

SHERIA NDOGO ZA USHURU WA HUDUMA ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA ZA MWAKA 2022

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo ya Ushuru wa Huduma za Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela za Mwaka 2022.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi itatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:

Afisa mwidhiniwa" maana yake ni mtumishi yeyote wa Halmashauri au mtu yeyote mwingine atakayeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela.

"Hesabu" maana yake ni jumla ya mauzo katika mwaka husika wa mapato;

"Hesabu za mwisho" maana yake ni taarifa za kihasibu zinazowasilishwa na mlipa ushuru baada ya kipindi cha hesabu kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, zikijumuisha nyaraka, hesabu au maelezo yoyote yahusuyo kiasi na thamani ya kifedha ya bidhaa au huduma zilizouzwa;



Scanned with CamScanner

"Kipindi cha hesabu" maana yake ni muda ambao mlipa ushuru atatakiwa kuwasilisha hesabu za mauzo yake;

'Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela au mtumishi yeyote atakayeteuliwa kwa wakati huo kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

"Mlipa ushuru" maana yake ni kampuni, tawi la kampuni au mtu mwenye leseni ya biashara anayefanya shughuli zake katika eneo la Halmashauri;

"Ushuru wa huduma" maana yake ni malipo yanayotolewa kwPPa Halmashauri kutoka kwa kampuni, tawi la kampuni au mtu mwenye leseni ya biashara iliyotolewa chini ya sheria yoyote kwa huduma za umma anazotumia kufanya biashara katika eneo la Halmashauri;

"Wakala" maana yake ni kampuni iliyoingia mkataba na Halmashauri kwa ajili ya kukusanya Ushuru wa Huduma.

Utozaji wa Ushuru

4.- (1) Halmashauri itatoza na kukusanya Ushuru wa Huduma kutoka kwa kila mlipa kodi ya Mapato na Mwenye leseni ya biashara kutoka Halmashauri.

(2) Ushuru utakaotozwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) utatozwa katika kila kipindi cha hesabu kwa kiwango cha asilimia sifuri nukta tatu (0.3%) ya mauzo ya bidhaa au huduma yanayofanyika katika eneo la Halmashauri baada ya kutoa Kodi ya Ongezeko la Thamani na Ushuru wa Bidhaa.

(3) Mfanyabiashara mwenye leseni ya biashara ambaye ameshindwa kutunza kumbukumbu na hakuna namna ya kupata taarifa zake atalipa ushuru wa huduma kwa kufuata viwango vilivyoonyeshwa kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.



Scanned with CamScanner

Ukaguzi wa kumbukumbu za biashara

5.- (1) Mkurugenzi, Afisa mwidhiniwa au Wakala anaweza katika muda wa kazi kuingia kwenye jengo au eneo la biashara la mlipa ushuru kwa nia ya kufanya ukaguzi na tathmini ya kumbukumbu za biashara, vitabu vya hesabu na taarifa nyingine kama atakavyoona inafaa kufanyiwa ukaguzi kwa ajili ya kujua kiwango sahihi cha ushuru kinachotakiwa kulipwa.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), Mkurugenzi anaweza, kwa notisi ya siku saba, kumtaka mlipa ushuru kuwasilisha kumbukumbu za kibiashara na vitabu vya hesabu, kwa nia ya kupata taarifa kwa ajili ya kufanya tathmini au kukusanya Ushuru wa Huduma.

(3) Kwa madhumuni ya utekelezaji wa masharti ya kifungu kidogo cha (2), Mkurugenzi anaweza kumtaka mlipa ushuru kufika mbele yake.

Muda wa kulipa

Sura ya 290

6. Bila kuathiri masharti ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa na sheria nyingine yoyote, kila mlipa ushuru atatakiwa kuwasilisha hesabu za awali na kulipa ushuru unaotakiwa katika kila kipindi cha miezi mitatu katika mwaka wa fedha wa Serikali.

Kuwasilisha hesabu za mwisho

7.- (1) Kila mlipa ushuru atatakiwa kuwasilisha kwa Halmashauri hesabu za mwisho katika kipindi cha miezi mitatu tangu kumalizika kwa kipindi cha hesabu.

(2) Mkurugenzi au Afisa mwidhiniwa anaweza-

(a) kukubali hesabu za mwisho na kutathmini ushuru katika msingi huo; au

(b) kukataa hesabu za mwisho na kufanya tathmini ya kuhusu hesabu hizo iwapo atakuwa na sababu za msingi za kuamini kuwa hesabu hizo siyo sahihi

(3) Iwapo mlipa ushuru hajawasilisha hesabu za mwisho kwa mwaka wa fedha husika na ametakiwa kufanya hivyo kwa notisi ya siku kumi na nne (14), Mkurugenzi au Afisa mwidhiniwa anaweza, kwa kadri atakavyoona inafaa, kuamua au kukadilia kiwango cha hesabu za mlipa ushuru huyo kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.



Scanned with CamScanner

(4) Ushuru uliotathminiwa kwa mujibu wa Sheria ndogo hizi utalipwa katika muda wa siku saba (7) tangu tarehe ya kufanya tathmini.

Makosa na adhabu

8.- (1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo-

(a) atashindwa kulipa ushuru wa huduma ndani ya muda ulioainishwa katika Sheria Ndogo hizi;

(b) atashindwa kuwasilisha hesabu sahihi kwa Halmashauri;

(c) atashindwa kutunza kumbukumbu yoyote au nyaraka kwa ajili ya ukaguzi; au

(d) atamzuia au atajaribu kumzuia Mkurugenzi, Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Mtu yeyote atakayetiwa hatiani kwa kosa lililoainishwa katika kifungu kidogo cha (1) atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili (Tsh 200,000/=) na isiyozidi shilingi milioni moja (1,000,000/=) au kutumikia kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au adhabu zote kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufililisha kosa

9. (1) Bila kuathiri masharti ya Sheria Ndogo hizi, Mkurugenzi anaweza kufililisha kosa kwa kutoza kiasi cha Shilingi Laki moja kwa mtu yeyote atakayekiri kutenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi na kuwa tayari kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Mtu atakayekiri kosa chini ya kifungu kidogo cha (1) atatakiwa kujaza fomu maalum iliyoainishwa kwenye Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.

TS Na. 279 la Mwaka 2019

10. Sheria Ndogo za Ushuru wa Huduma za Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela 2019 zimefutwa.



Scanned with CamScanner

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4 (3))*

### USHURU WA HUDUMA KWA WAFANYABIASHARA WASIOTUNZA KUMBUKUMBU

| Na. | Kiwango cha Ada ya Leseni ya Biashara kwa mwaka | Malipo ya Ushuru wa Huduma kwa mwaka |
|---|---|---|
| 1. | 1 - 50,000/= | 30,000/= |
| 2. | 50,001/= - 100,000 = | 50,000/= |
| 3. | 100,001/= - 200,000/= | 70,000/= |
| 4 | 200,001/= -300,000/= | 100,000/= |
| 5 | 300,001 -500,000/= | 130,000 = |



Scanned with CamScanner

## JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 9 (2))*

## FOMU YA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ..................................................... mwenye namba ya simu.................................... Wa S.L.P ...................... Ninaefanya Biashara ya ........................... Katika eneo la .................................. lililopo katika eneo la mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kwa hiari yangu mwenyewe nakiri kuwa Tarehe ......... Mwezi ............. Mwaka ................. nilikiuka aya ya ..........................ya Sheria Ndogo ya Ushuru wa Huduma ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela za Mwaka 2022.

Kwa hiyo, kwa hiari yangu mwenyewe na bila kushurutishwa na mtu yoyote nakubali kulipa kiasi cha Tsh............................... badala ya kushitakiwa Mahakamani na nipo tayari kutimiza wajibu wangu iwapo Mkurugenzi ataamua kutekeleza madaraka yake aliyopewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Jina: ..........................................................................

Saini: ....................................... Tarehe: ...........................

MBELE YANGU:

Jina: ...........................................

Saini:.......................................

Wadhifa: ..................................

Tarehe: ....................................



Scanned with CamScanner

Nembo ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela imebandikwa kwenye sheria ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa katika kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kilichofanyika tarehe 10/09/2022.

Eng. MODEST JOSEPH APOLINARY,
*Mkurugenzi wa*
*Halmashauri ya Manispaa*
*Ilemela*

MH. RENATUS BAHEBE MULUNGA
*Mstahiki Meya wa Halmashauri ya Manispaa*
*Ilemela*

L.S

NAKUBALI

INNOCENT L. BASHUNGWA
*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais,*
*TAMISEMI*

*Dodoma*
23/6/2022



Scanned with CamScanner